JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA

# SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA

ISO 9001:2015 Certified

*Mwanachama wa Shirika la Viwango la Kimataifa (ISO), Codex Alimentarius Commission (WHO/FAO) na Wakala wa ISO na Mashirika ya Viwango ya Mataifa mbalimbali*

## TAARIFA KWA WAAGIZAJI, WASAMBAZAJI NA WAUZAJI WA NGUO ZA MITUMBA

**Dar es Salaam, 02 Julai 2025**

Hivi karibuni katika kaguzi zinazoendelea sokoni, Shirika la Viwango Tanzania (TBS) lilikamata bidhaa za nguo za mitumba zilizopigwa marufuku. Hii inatokana na uwepo wa baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu wanaoingiza nguo hizo kupitia njia zisizo rasmi na kuendelea kuuza na kuzisambaza. Nguo hizo ni pamoja na nguo za ndani, taulo, soksi, barakoa, nguo za hospitalini, leso, nguo za kuakisi mwanga (reflectors) na nguo zote zinazoendana na hizo ambazo zinaweza kuleta madhara ya kiafya au kusambaza maradhi zinapotumika.

TBS inawakumbusha waagizaji, wasambazaji na wauzaji wa nguo za mitumba kuzingatia matakwa ya Sheria ya Viwango Sura ya 130 na Kanuni zake, pamoja na Kiwango cha Kitaifa cha nguo zilizotumika (nguo za mitumba), TZS 758:2023/EAS 356:2019, ambacho kinakataza uagizaji, uuzaji au usambazaji wa bidhaa hizo.

TBS itaendelea kuhakikisha kuwa, matakwa ya Sheria kuhusiana na ubora na usalama wa bidhaa za nguo za mitumba yanazingatiwa na wadau wote ili kuepuka athari za kiafya zinazoweza kujitokeza kwa wananchi.

Kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana nasi kupitia namba ya bure **0800110827.**

**Imetolewa na;**

Gladness H. Kaseka
**Meneja wa Uhusiano na Masoko**


**TBS MAKAO MAKUU**
Shirika la Viwango Tanzania
Barabara ya Sam Nujoma / Morogoro, Ubungo, Dar es Salaam
S. L. P. 9524
DAR ES SALAAM, TANZANIA
Simu Na: +255 22 245 0298/ +255 22 245 0206
Nukushi: +255 22 2450959
Namba ya Simu Bila Malipo: 0800110827
Barua pepe: info@tbs.go.tz
Tovuti: http://www.tbs.go.tz
Barua pepe kwa ajili ya malalamiko ya wateja: malalamiko@tbs.go.tz
Twitter: TBS_Tanzania
Instagram: tbs_Viwango

**TBS KANDA YA KATI**
Jengo la Kambarage
S. L. P. 2956
DODOMA, TANZANIA
Simu Na: +255 26 2520310

**TBS KANDA YA ZIWA**
Jengo la NSSF, Ghorofa ya 3
S. L. P. 1814
MWANZA, TANZANIA
Simu Na: +255 28 2505044

**TBS KANDA YA KASKAZINI**
Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2
S. L. P. 2399
ARUSHA, TANZANIA
Simu Na: +255 27 2520143

**TBS KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI**
Jengo la NHIF, Ghorofa ya 7
S. L. P. 1674
MBEYA, TANZANIA
Simu Na: +255 25 2502848

**TBS KANDA YA KUSINI**
Jengo la MTUWASA
S. L. P. 1396
MTWARA, TANZANIA
Simu Na: +255 23 2334477

**TBS KANDA YA MAGHARIBI**
Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2
S. L. P. 1276
KIGOMA, TANZANIA
Simu Na: +255 28 2804023